

DHIHIRISHO LA UKWELI

NA

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,
Masihi Aliyehadiwa na Imam Mahdi a.s.

Wafasiri

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani
na Sheikh Faiz Ahmad Zahid

**JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA**

Dhihirisho la Ukweli

Tafsiri ya Kiswahili ya *Sachchā`ī kā Idh-har*

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1893

Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2009

Nakala: 2000

Kimeenezwa na:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania

Mnazi mmoja, Dar es Salam.

Simu: +255222110473

Fax: +255222121744

Kimechapwa na:

Ahmadiyya Printing Press

Dar es Salam, Tanzania

Simu: +255222111031

ISBN 9987 - 438 - 12 - 1

FAHARISI

DIBAJI	1
Maelezo ya msaada dhahiri uliowafikia mapadre katika mambo ya dini kutoka kwa "Isha-atus-Sunna" la Sheikh Muhammad Husain wa Batala.	3
Tangazo kwa wote	6
Kuondoa wasiwasi mmoja wa Daktari Martyn Clark	7
Ushahidi wa mtaalamu mmoja mwarabu ambaye ni mwalimu wa kufundisha elimu za fasihi katika mji mmoja mkubwa, kuhusu ufasaha wa hali ya juu wa kitabu changu " <i>Aina Kamalate Islam</i> " na " <i>Tabligh</i> "	9
Barua ya upendo ya mtaalamu mwarabu kwangu.	10
Jibu la barua ya upendo ya mtaalamu mwarabu kutoka kwangu	12
Barua ya mtaalamu mmoja mwarabu wa Makkah	15
Muhtasari wa barua ya mtaalamu mmoja wa Kiarabu Seyyid Ali bin Sharif Mustafa mwarabu	16
Ahadi ya Bwana Abdallah Atham, Wakili wa Daktari Martyn Clark, na Wakristo wengine kusilimu wakishindwa.	17
Nakala ya barua ya Bwana Abdallah Atham kutoka Amritsar ya 9 Mei 1893.	18
Tangazo la Mubahala kwa kujibu tangazo la Abdul Haki Ghaznawii	19
Kukamilisha hoja	22

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DIBAJI

Sayidna Ahmad a.s., Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, aliandika kijitabu hiki '*Sachchai ka Idh-har*' (Dhihirisho la Ukweli) katika mwezi wa Mei 1893. Ndani yake aliwakaribisha mapadre kujadili juu ya ukweli wa dini ya Kiislam. Vile vile aliwaita Masheikh wa jina kwa ajili ya mubahala. Ilhali Masheikh na wanazuoni wenye nuru ya imani na elimu walikuwa pamoja na Sayidna Ahmad a.s. Alivyoandika kwamba "Wanazuoni wote wa Kiislamu wanaotegemewa ambao Mwenyezi Mungu Amewajaalia elimu na amali na kuwapa nuru ya imani, wako pamoja nami wakati huu ndio takriban arubaini. Lakini watu wa kundi la pili wengi wao ni Masheikh wa jina tu wasio na sifa bora za ujuzi wa amali." uk.7

Kijitabu hiki kiliandikwa katika lugha mbili, Kiurdu na Kiarabu. Sehemu ya Kiurdu imefasiriwa na Sheikh Faiz Ahmad Zahid na sehemu ya Kiarabu imefasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani.

Tafsiri hii iliboreshwa na Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, akisaidiwa na Sheikh Mubarak Mahmud. Vile vile katika kukamilisha kazi hii Bwana Muhammad Shafiq Sehgal na Bwana Sharifu Tanwir Mujtaba

wakasaidia kwa njia mbalimbali. Tafsiri hii pia ni tunda la 'Deski ya Kiswahili'.

Wafasiri na wote walioshughulikia kazi hii kubwa wanastahili kuombewa. Mwenyezi Mungu awajaalie malipo bora na akubali juhudi na huduma yao. Amin.

Ch. Muhammad Ali M.A.

Wakilut Tasnif,

Tahrike Jadid, Rabwah,

Pakistan.

28/12/2008

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ¹

**Maelezo ya msaada dhahiri uliowafikia mapadre
katika mambo ya dini kutoka kwa "Isha-atus-Sunna" la
Sheikh Muhammad Husain wa Batala.**

Katika "Kiwanda cha Uchapishaji cha Misheni ya Marekani", Ludhiana, limechapwa tangazo moja dhidi yangu, tarehe 12 Mei 1893, kutoka kwa Daktari Henry Martyn Clark M.D., Mishonari-Daktari wa Amritsar, ambamo kwa namna fulani imetolewa shukurani kwa Sheikh Muhammad Husain ajulikanaye kuwa Sheikh mkazi wa Batala. Na kwa kweli Wakristo walikuwa na sababu ya kutoa shukurani, kwani Bwana Daktari japo alikubali kufanya mjadala nami kwa kuchambua na kuhakiki Islam na Ukristo, na kuchunguza haki na batili, lakini halafu baada ya kutafakari akatawaliwa na hali ya kutisha. Ni kweli kwamba mwanadamu afanywapo kuwa Mungu, wakati wa kulinganisha mwili unatetemeka. Mungu ni Mungu na mwanadamu ni mwanadamu; kuna mlingano gani kati ya vumbi na

¹ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Wake Mtukufu.

Mweza Mtukufu! Ilmuradi, mapadre walipohofia isije siri ya mpango wa Kikristo ikatobolewa ukilinganishwa na njia iliyonyoka ya Islam, wakaonelea ifanywe juhudi ili mjadala huu afadhali uahirishwe, na kama kikombe hiki kiwaepuke ni bora zaidi. Katika hali hii ya hamu na ghamu wakapata msaada mkubwa kutoka kwa Bwana Sheikh. Huenda Bwana Sheikh mwenyewe aliwaandea mapadre kisirisiri, kwa shabaha ya kuwasaidia; kwani ile barua aliyoniandikia Bwana Daktari na ameandika baadhi ya maandiko ya *'Isha-atus-Sunna'*, hayo yanafanana sana na maandiko ya Bwana Sheikh. Iwapo aulizwe Sheikh kwa kula kiapo, pengine hatakataa. Kisha kile kiambatisho cha *'Nur Afshan'* kilichochapwa tarehe 12 Mei 1893 na kipo mikononi mwangu hivi sasa, tukikiangalia kwa makini hicho nacho kinatoa ushahidi. Haya ndiyo maneno yake: Nyinyi (enyi wakazi wa Jandiala) mnatuletea mzee (yaani mimi mnyeyekevu) kujadiliana naye ambaye kwanza hata kumfikiria kuwa Mwislamu ni shida. Mnahangaikia mawazo gani? Je hamkuona zile fatuwa zilizoenezwa na Maulamaa wa Kiislamu wa Panjab na India kumhusu Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian? Hao wanaandika katika fatuwa hizo kwamba yote tuliyosema kujibu swali la muulizaji na kutoa fatuwa kumhusu Mkadiani, ni sahihi, na Kitabu na Sunna na kauli za Maulamaa wa Kiislamu ni mashahidi juu ya usahihi wake. Waislamu wote wanapaswa wajiepushe na dajjal na mwongo kama huyo

na wasitendeane naye mambo ya dini yanayopaswa kuwa baina ya Waislamu wala wasisuhubiane naye, wala wasitangulie kumtolea salamu, wala wasimwalike katika karamu ya Suna, wala wasikubali mwaliko wake, wala wasisali nyuma yake, wala wasimsalie sala yake ya jeneza. Yu mwizi wa dini, anazidisha maradhi; ni dajjali, mwongo sana, mlaaniwa, hana dini, ametoka katika Islam, kafiri bali kafiri mkubwa kabisa, najisi, laghai, aliyepotezwa na Ibilisi na anayewapoteza wengine, ametoka katika Usuni; dajjali mkubwa sana bali ni ami wa dajjali, anayechuma dunia kwa kutumia dini. Ikiwa mnataka maelezo zaidi, basi mnaweza kujionea wenyewe kwa kuagiza kitabu '*Isha-atu-Sunna Annabawiya*' kutoka kwa Bwana Sheikh Abu Saidi Muhammad Husain, bei yake rupia moja na anna nane; chapatikana Lahore. Mmeghafilika kiajabu kwamba mpaka sasa hamjakiona kitabu hicho. Shabashi kwenu na kwa hima ya Waislamu wa Jandiala kwa kumfanya kuwa kiongozi yule ambaye hata kumsalia jeneza lake hairuhusiwi. Lo, masalale!!

Sasa yapasa iangaliwe kwa makini kwamba Bwana Padre amefaidikaje kutokana na Bwana Batalwi na '*Isha-atu-Sunna*'lake, na wanikufurishao wamewapatia nafasi gani wapinzani (wa Islam)! Lakini ni jambo la furaha kwamba baada ya kupata barua hii yenye fitina iliyonukuliwa kutoka katika '*Isha-atu-Sunna*', Wajandiala wenye imani thabiti hawakuyumba hata

kidogo, na Bwana Muhammad Bakhsh toka Jandiala akawatolea mapadre jawabu la kuwanyamazisha. Akaandika kwamba hakuna dini yoyote isiyo na hitilafu ndani yake. Hata Wakristo hawakuepukana na hali hii. Nasi tunawaona masheikh wa aina hiyo wenyewe ni wafisadi ambao wanamwita Mwislamu ambaye ni msaidizi wa Islam kuwa kafiri.

Tangazo kwa wote

Sheikh wa Batala wa '*Isha-atu-Sunna*' alitoa ahadi madhubuti mara mbili kwamba tarehe fulani na fulani lazima atatuma majibu ya barua ile iliyoandikwa kutoka upande wetu ili kutimiza hoja, kuhusiana na maelezo katika Kiarabu na kasida kushindana nami, wala hatafanya kinyume, lakini sasa siku kumi na sita zimekwisha pita baada ya tarehe hizo mbili, na Mungu Anajua bado siku ngapi zitaendelea kupita. Kuahidi kwake Sheikh mara kwa mara na kuivunja inaonyesha wazi kwamba sasa anasumbuliwa na taabu fulani. Siku tatu zimepita nilipata ujumbe kwa muhtasari kutoka Amritsar kwamba baadhi ya masheikh wanasema kwamba kama ingejadiliwa uhai na kifo cha nabii Isa katika mdahalo huu, sisi tungeungana na Dkt. Martyn Clark. Kwa hiyo, Bwana Sheikh na marafiki zake

wanaarifiwa, bali wanaapishwa, wao watoe hasira yao. Lazima mjadala utafanywa na Dkt. Clark na kuhusu uhai na mauti ya Nabii Isa (a.s.); msaidieni tu yeye bila wasiwasi. Na jueni kwamba Mungu Atawafedhesha waongo. Na mwito wetu wa mwisho ni kwamba sifa zote njema zamhusu Mola wa wailmwengu.

Kuondoa wasiwasi mmoja wa Daktari

Martyn Clark

Bwana Daktari katika kipeperushi chake cha tarehe 12 Mei 1893 kilichochapwa kama kiambatisho cha Nur Afshan la Ludhiana amedanganyika kutokana na gazeti la *'Isha-atu-Sunna'* la Sheikh wa Batala au ametaka kuwadanganya watu kana kwamba wanazuoni wa Kiislam wananikufurisha. Kwa hiyo yaandikwa kwa kuwafahamisha wote kwamba wanazuoni wote wa Kiislamu wanaotegemewa ambao Mwenyezi Mungu Amewajaalia elimu na amali na kuwapa nuru ya imani wako pamoja nami na wakati huu ndio takriban arubaini. Lakini watu wa kundi la pili wengi wao ni Masheikh wa jina tu wasio na sifa bora za ujuzi wala amali. Kama kauli yangu hii si ya kukuza jambo kwa Bwana Daktari, basi Bwana Daktari ashiriki mwenyewe katika mjadala wowote utakaofanyika baina ya

Maulamaa wapinzani na Maulamaa wenye ujuzi wa Jumuiya yangu. Bali hivi karibuni, hadi tarehe 15 Juni 1893, kutakuwa na mkutano wa mjadala ambamo kundi la mpinzani Sheikh Ghulam Dastaghir na Maulamaa wenzake wote wa Lahore watakuwepo na kutoka upande wetu mtalaamu mmoja au wawili watapendekezwa kujadiliana, kisha Bwana Padre ataweza kushuhudia mwenyewe kwamba Maulamaa wamchao Mungu na wataalamu halisi wapo upande gani, na maulamaa wa jina tu na wenye mazungumzo ya matata-matata wapo upande gani. Kuna msemo maarufu kwamba "kusikia si sawa na kuona." Maneno yanayotoka katika kalamu ya adui bahili kwa kupendelea upande mmoja hayawezi kuwa na uzito wala heshima machoni mwa wenye akili, bali kila hakika hufunuka wakati wa jaribio.

Zaidi ya hayo, Bwana Daktari anajua pia kwamba makao makuu ya wanazuoni wa Kiislamu ni miji miwili mitakatifu; Mwenyezi Mungu Aizidishie utukufu, heshima na baraka; na katika Islam nchi hii ya Uarabu, hususan Makkah na Madina, huhesabiwa kuwa makazi ya dini. Basi wanamiji na wanazuoni wa mahali hapo patakatifu pia wanaendelea kuungana nami. Hivyo, naandika hapa chini maandishi ya wazee watatu kama ni mfano.

**Ushahidi wa mtaalamu mmoja mwarabu
ambaye ni mwalimu wa kufundisha elimu za fasihi
katika mji mmoja mkubwa, kuhusu ufasaha wa hali
ya juu wa kitabu changu "*Aina Kamalate Islam*" na
"*Tabligh*"**

Ndugu yangu Maulawii Hafidh Yakubu, Mungu Amweke salama, anaandika kutoka Deraduni kwamba: Ninaamini kwamba u Imamu wa zama hizi, wasaidiwa na Mwenyezi Mungu. Mungu Amewafanya Maulamaa kuwa mawindo yako au watumwa wako. Mpinzani wako hatafanikiwa kabisa. Mwenyezi Mungu Aniweke hai nikiwa miongoni mwa watumishi wako na Anifishe katika hali hiyo. Ee Mungu, Ufanye hivyo. Mwanachuoni mmoja Mwarabu amekaa nami wakati huu. Yu Msiria, Sharifu, mwandishi mkubwa, amehifadhi maelfu ya beti za Waarabu halisi. Nikaongea naye juu yako. Yu mtaalamu mkubwa na mimi mtu wa kawaida kabisa, lakini kuhusu maana ya "tawaffa" hakuweza kufua dafu. Akaonyeshwa maandiko yako ya '*Aina Kamalate Islam*' yaliyo kwa Kiarabu, akasema: Wallahi, Mwarabu hawezi kuandika hivi sembuse Mhindi: Nikamwonyesha kasida ya kumsifu Mtume s.a.w. Akiisoma akalia na kasema, Wallahi, sikupenda katu beti za Waarabu wa zama hizi sembuse beti za Wahindi; lakini beti hizi nitazihifadhi. Na akasema,

"Wallahi, yeyote atakayedai kuandika maandiko bora zaidi kuliko haya, hata akiwa Mwarabu, yu maluuni Musailamah mwongo kabisa." Maneno yake yamekwisha. Mimi nina yakini kwamba huu ni mwujiza wa Neno la Mungu na msaada wake; si kazi ya mwanadamu. Mimi nimekufanya mmiliki wa uhai wangu na wa ahali na watoto wangu.

Barua ya upendo ya mtaalamu mwarabu kwangu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Ewe yule ambaye upepo mwanana wa shauku unajitafutia sifa njema kutoka kwako, na maua ya nargisi yanapata harufu nzuri na manukato kutoka kwa uturi wako, dhati yako tukufu imezungukwa na siri za ndani kabisa, na dhati yako yenye baraka ya hali ya juu imehifadhiwa dhidi ya masaibu ya kadiri. Safina zako za kuokoa zaendelea kupita katika bahari za elemu. Na bendera zako za kutatua matatizo kuhusu maana yenyewe ya maneno na muradi wake ziendeleo kupepea. Vipaji viendeleo kusujudu mbele ya cheo chako kikubwa na aali. Na midomo iendeleo kuwa mashahidi kusifu sifa na uzuri wa dhati yako. Kukusifu kwangu, kukuombea na shauku yangu na kuonana nawe haielezeki. Asslamu alaikum warahmatullahi

wabarakatuhu. Hayo ndiyo maamkizi kutoka kwa mapenzi thabiti na moyo usiochafuka na uchafu wote. Ama baadu, upepo mwanana wa matarajio ukamvumia mwandishi, na shauku kubwa ya kuhama ikamchochea, na kadiri ya Mungu ikamleta katika mji mmoja wa nchi hii, na kwa kadiri ya Mmiliki Mwumbaji Mkuu, bahati njema ikamkutanisha na ndugu mpole na rafiki mwenye huruma, Hafidhi Sheikh Muhammad Yakub– Mungu amlinde na matope ya aibu na mashimo ya madhambi – katika eneo la Deraduni; eneo lake liendelee kujaa daima upaji wa Mungu. Tulianza kupata taarifa na tukakumbushana kumbukumbu la zama na hali zilizopita na kutangulia mpaka mazungumzo yakatufikisha katika zama hizi. Basi ukatajwa wewe mheshimiwa. Ndipo nikamwuliza maelezo na ufafanuzi zaidi kukuhusu wewe. Naye akanipasha habari zako na sifa zako nzuri ipasavyo, hadi fikara yangu na moyo wangu ukapatwa na hamu sana ya kukuona niliposikia baadhi ya sifa zako njema. Maana mazungumzo hueleza sifa ya mzungumzaji, na haikufichikana ile faida iliyomo katika kuonana ana kwa ana; kwa hiyo Hadhrat Musa a.s. akataka kuonana (na Mungu). Hakuna kilichonizuia isipokuwa matatizo ya njiani, joto kali, mikono mitupu, mfuko usio na kitu, ukosefu wa njia ya usafiri. Kama ningeweza kuruka, ningeruka kwa shauku kukufikia; wala nisingerudi nyuma kabisa. Lakini mabawa yangu yamekatwa; na mwenye kukatwa ubawa

awezejaje kuruka? Kwa vyovyote kama hiyo hiwezekani kwa miguu, lakini yawezakana kwa kalamu, hususan kuna msemo: Kalamu ni ulimi mmojawapo katika ndimi mbili. Na barua ni nusu ya kuonana. Lakini kusikia si kama kushuhudia, kwani huku ni kuona kwa jicho la yakini; isipokuwa tukosapo maji tunaelekea kwenye badili yake. Wassalamu.

Jibu la barua ya upendo ya mtaalamu mwarabu kutoka kwangu

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ²

Amma baadu, ujue, ewe unipendaye na mwenye ikhlasi kwangu, kwamba barua yako tukufu imeniwasilia. Nilipoifungua na kuiangalia na kusoma na kufahamu yaliyomo humo, lo hiyo ilikuwa kutoka kwa mpenzi mtambuzi na mtawa, fahamivu na mwenye akili na mhakiki mwenye busara, mwenye rai iliyo sawa na akili pevu, kwangu mimi mnyenyekevu, ninayefanywa shabaha ya kukufurishwa, niachwaye na kila mdogo na mkubwa. Basi nikamshukuru Mungu kwa kunipatia mpenzi kama wewe na mfariji kutoka miongoni mwa

² Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Wake Mtukufu.

Waarabu halisi. Na alinipatia habari njema ya mapenzi ya wahishimiwa hao. Nami nitatunga kitabu kimoja kwa kupeleka nchi za Waarabu na Shamu, huenda nikasaidiwa na wahishimiwa hao. Basi nikapokea barua yako katika siku ya baraka sana. Nikaihesabu kuwa ni tunda la kwanza miongoni mwa matunda ya Uarabuni na nimeichukulia kama fali njema kwa kurekebisha mashariki na magharibi. Na moyo wangu ukawa na shauku kwamba Mwenyezi Mungu anipeleke katika nchi yako ili nifaulu kuonana nawe. Ee ndugu yangu! Maulamaa wa nchi hii wamenikufurisha na kunikadhibisha na kunisingizia kwa masingizio mengi na kunishambulia wakinilaani na kunikebehi na kutumia lugha chafu. Nami nimejitenga kabisa na maulamaa hao na elimu yao. Na nimejiunga na wale wanaoshuku Uislamu wao. Naona mioyo yao yafanana na mioyo ya Wayahudi katika kudhania vibaya kwa kujasiri mbele ya Mola Mwabudiwa. Wanag'ang'ania kunikufurisha na wamejitahidi kuiniudhi. Na wamemkufurisha mumini amwaminiye Mungu Mmoja katika maandishi na mazungumzo yao. Na hawakujuta katika kuharakia kukufurisha na wakadhani kwamba wakati huu sio wakati wa kudhihiri Mujaddidi ambaye atajadidisha dini na kuwafukuzilia mbali mashetani. Je hawakuona kwamba giza limetapakaa na njia ya wema imefichikana kabisa. Na adui ameishambulia ngome ya Islamu na kuiba. Na giza limechukua nafasi ya nuru na

limeipoteza. Na ile kaumu imeishinda ardhi ambayo inaabudu msalaba na kumfanya mtu dhaifu na masikini kuwa mwabudiwa, na inampoteza wa mbali na wa karibu. Mikononi mwao hakuna kitu isipokuwa hila, uwongo au mali nyingi na vipofu na chongo wanaelekea kwao na makundi na umma wameingia katika wavu wao. Inawezekana maangamizi haya yawafikie Waislamu wengi, nao wanaangamia kwa mikono ya wadanganyifu. Basi Mwenyezi Mungu Aliona ummati huu uliopaswa kuhurumiwa na Akawakuta ni dhaifu, ndipo Akamtuma mtumishi kutoka miongoni mwa watumishi wake kwa kujadidisha dini na kushindisha hoja. Ee ndugu yangu, siku hizi ni kama usiku wa kiza na njia ya kuhilikisha. Mwenyezi Mungu Akaona fisadi za zama hizi na fitina za zama hizi kutapakaa na giza la kufuru na uasi na viumbe ukiongoni mwa moto, basi akawapatia kwa fadhili zake taa ambayo inawakinga na kujikwaa na inanururisha Sunna na Hadhiti. Nimekueleza baadhi ya mambo haya machungu ili uhurumie hali dhaifu ya Islam, kwani nakunona kijana mwema na miongoni mwa wenye ikhlasi na upendo. Umenifurahisha kwa maneno ya mahaba yako. Na umemfariji kwa kauli za upendo wako maskini huyu aliyeachwa na umma na kukebehiwa na kulaumiwa. Basi, Mungu Akupatie malipo na

Akurehemu, naye ndiye Mrehemevu zaidi kuliko wanaorehemu. Amin.

Mwandishi, Mtumishi dhaifu aliyeachwa na kaumu,
Ghulam Ahmad, *Mungu Amrehemu*.

Barua ya mtaalamu mmoja mwaarabu wa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Sifa zote njema zamhusu Mungu, Mola wa walimwengu. Baraka na amani ziwe juu ya mbora wa viumbe vyote (Mtume Mtukufu s.a.w.).

Kwa janabi mhashamu, muadhamu, mtukufu, mkarimu, maulana, Imamu wetu, kiongozi wetu na Masihi wa zama zetu, Ghulam Ahmad, Mwenyezi Mungu Amhifadhi. Amin thuma amin, Ee Mola wa walimwengu.

Amma baadu, Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu. Barua yako tukufu imetuwasilia na tumeisoma na kuelewa yaliyomo humo na tumemhimidi Allah kwamba m kwa heri na afya. Ee hababi wangu, namuomba Mungu kisha wewe gofira na msamaha kwa makosa niliyofanya. Hababi wangu, mimi ni mwanao na

hadimu wako, nawajibika kuulizwa na Mungu na wewe. Nimetubu na nimeahidi kwamba, Mungu akipenda, sitarudia abadan wala sitasema katu mithili ya maneno yaliyotajwa. Mwenyezi Mungu aboreshe hali zako na Athamini fadhila yako. Wassalamu, Mwandishi, mtumishi hakiri, Mahmamad bin Ahmad wa Makkah.

Maneno uliyoyaandika katika barua yamenipendeza. Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu ambaye Ameniahidi kukutana nawe. Hakuna shaka wala wasiwasi kwamba u kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tumeamini na tumesadikisha. Na kauli yetu ya mwisho ni kwamba sifa zote njema zamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.

Mwandishi,

Muhammad bin Ahmad wa Makkah.

Muhtasari wa barua ya mtaalamu mmoja wa Kiarabu Seyyid Ali bin Sharif Mustafa mwarabu

Bwana Seyyid Mwarabu ameandika katika barua yake ndefu beti nyingi kama kasida ya kusifu na nathari ndefu kama kusifu na kutukuza. Miongoni mwa maandishi yake mengi kuna maandiko haya pia:

Kwa janabi, mwadhamu, mhakiki mwenye busara, jabali ya akili nyingi, nyota inayong'aa ya mashariki, thabiti, mtume wa Mungu Adhimu, mpokeaji wa funuo, nguzo ya dola la milele, sultani wa raia ya Kiislamu, Mirza Ghulam Ahmad – fadhili zake zinang'aa kama nyota katika nchi za mbali kwa kila jahili na mwenye akili – bahari ya ukarimu ambayo ukingo wake hauonekani; na ni chanzo cha chemchem ya elimu na ukarimu ambavyo vituo vyake penye maji ni safi.

Ni tumaini kwamba wakati mwingine kasida na barua kamili ya mtaalamu mwarabu itachapishwa. Kwa hivi sasa kama ushahidi hiyo inatosha.

**Ahadi ya Bwana Abdallah Atham,
Wakili wa Daktari Martyn Clark, na
Wakristo wengine kusilimu wakishindwa.**

Wakati huu twaandika hapa chini ile ahadi ya Bwana Abdallah Atham Extra Assistant wa zamani na sasa anapata pensheni, mtemi wa Amritsar, aliyoifanya akiwa wakili wa Dkt. Martyn Clark na Wakristo wengine wa Jandiala, kusilimu wakishindwa. Bwana Huyo mtajwa

amekubali waziwazi katika barua yake ya ahadi kwamba akishindwa katika majadiliano ya maana au kuona mwujiza basi atasilimu na ahadi yake ndiyo ifuatayo:

Nakala ya barua ya Bwana Abdallah Atham

kutoka Amritsar ya 9 Mei 1893.

Mheshimiwa Mirza Ghulam Ahmad, Mkuu wa Qadian, kwa kujibu kitabu cha '*Hujjatul Islam*' ulichoandika kunihusu mimi nasema kwamba kama wewe au mtu mwingine yeyote akithibitisha kwa njia yoyote, yaani kwa kuonyesha mwujiza au kwa hoja thabiti ya kiakili kwamba mafundisho ya Kurani yanawezekana na kulingana na sifa tukufu za Mungu, basi nakiri kwamba nitasilimu. Mheshimiwa, uwe na uhakikisho wangu huu wa kimaandishi mikononi mwako. Kilichobaki ni kwamba unisamehe kwa kutotangaza magazetini.

Sahihi ya

Bwana Abdallah Atham.

**Tangazo la Mubahala kwa kujibu
tangazo la Abdul Haki Ghaznawii**

Tarehe 26 Shawali 1310 Hijriya

Nimewahi kuona tangazo la Mubahala la tarehe 26 Shawali 1310 lililotolewa na Abdul Haki Ghaznawii. Hivyo, natoa tangazo hili kwamba nakubali kufanya mubahala na huyu Bwana na kadhalika na kila mkufurishaji ambaye anaitwa mtalaamu au Sheikh. Nami natarajia, Mungu Mweza Akijaalia, nitafika Amritsar hadi tarehe tatu au nne ya Dhilkaadi 1310 na tarehe ya mubahala imewekwa kuwa 10 Dhilkaadi au kama ikinyesha mvua au ikitokea sababu nyingine ya muhimu, 11 Dhilkaadi 1310 Hijriya. Na tarehe hiyo haitaahirishwa kabisa. Na mahali pa kufnaya mubahala pamekubaliwa kuwa eneo la kusalia Idi lililo karibu na msikiti wa marehemu Khan Bahadur Muhammad Shah. Na kwa vile katika sehemu ya kwanza ya mchana mpaka karibu saa sita nitajadiliana na Wakristo juu ya ukweli wa Islamu na mjadala huu utaendelea kwa siku kumi na mbili mfululizo, kwa hiyo wenye kunikufurisha ambao wanataka kufanya mubahala nami, wanafahamishwa kwamba kuanzia saa nane mpaka jioni nitakuwa na nafasi. Katika nafasi hiyo, tarehe 10 Dhilkaadi au kwa sababu ya udhuru wowote tarehe 11

Dhilkaadi wafanye mubahala nami. Na sababu ya kupanga tarehe 10 Dhilkaadi ni kwamba ili maulamaa wengine wanaonikufurisha mimi nitoaye Shahada mbili na kuelekea Kibla katika sala, wao nao waweze kushiriki katika mubahala huu ambao kati yao kuna Muhyiddin wa Lakhu na Sheikh Abdul Jabbar na Sheikh Muhammad Husain wa Batala na Munshi Sadullah mwalimu wa shule ya Sekondari ya Ludhiana na Abdul Aziz Waidh wa Ludhiana na Munshi Muhammad Umar mfanyakazi wa zamani wa Ludhiana na Sheikh Muhammad Husain mtemi wa Ludhiana na Mian Nadhir Husain wa Delhi na Pir Haidar Shah na Hafidh Abdul Mannan wa Wazirabad na Mian Abdullah Tonki na Sheikh Ghulam Dastagir Kasuri na Sheikh Shahdin na Sheikh Mushtak Ahmad, mwalimu wa shule ya Sekondari, wa Ludhiana na Sheikh Rashid Ahmad Gangohi na Sheikh Muhammad Ali Waidh mkazi wa Bopran wilaya ya Gujranwala na Sheikh Muhammad Isihaka na Suleiman wakazi katika ufalme wa Patiala na Dhuhurul Hasan, mrithi wa sufii wa Batala na Sheikh Muhammad, mfanyakazi katika kiwanda cha uchapaji cha Karim Bakhsh, Lahore na wengineo. Kama watu hao baada ya kuwafikia matangazo haya yaliyotumwa kwa regista hawatafika katika uwanja wa Mubahala, basi hiyo itakuwa dalili imara kuthibitisha kwamba wanajijua wa waongo, wadhalimu, si wakweli katika itikadi yao ya kunihesabu kuwa kafiri. Hususan kwanza

kabisa Sheikh Muhammad Husain wa Batala, mhariri wa '*Isha-atus-Sunna*' anawajibika kufika Amritsar uwanjani kwa mubahala katika tarehe iliyowekwa, kwa sababu yeye mwenyewe ameomba kufanya Mubahala. Na ikumbukwe kuwa sisi hatutaki kufanya mubahala mara kwa mara, kwani Mubahala si mzaha wala mchezo. Wakufurishao wote wapaswa kuamuliwa hivi sasa. Kwa hiyo, baada ya kuenezwa tangazo letu mtu yeyote atakayekwepa na hatafika katika tarehe iliyopangwa, basi mtu huyo hatakuwa na haki tena ya kuleta ombi la Mubahala; na atakuwa hana haya kama ataendelea kuniita kafiri huko na huko nisipokuwepo. Matangazo haya yanatumwa kwa njia ya rejista kwa kukamilisha hoja, ili baadaye wanikufurishao wasibakie na udhuru wowote. Kama baada ya hapo wakufurishao hawatafanya mubahala wala hawataacha kunikufurisha, basi kutoka kwetu hoja itakuwa imetimia juu yao. Mwishowe ikumbukwe pia kwamba kabla ya mubahala tutakuwa na haki ya kueleza sababu za sisi kuwa Waislamu katika mkutano wa hadhara mbele ya watukufurishao. Amani iwe juu ya yule afuataye mwongozo.

Mtangazaji

Mirza Ghulam Ahmad

30 Shawali, 1310 Hijria.

Kukamilisha hoja

Sheikh Muhammad Husain wa Batala asipohudhuria tarehe 10 Dhilkaadi 1310 Hijiria, kwa ajili ya mubahala, basi tangu siku hiyo itafahamika kwamba imekwisha timia bishara iliyochapishwa kumhusu yeye kwamba atatubu kuniita kafiri.

Mwishoni naomba: Ee Mola Mweza, Umlaani huyo mdhalimu, mkaidi na mfitini na umdhalilishe kama baada ya mwito huu wa mubahala na kupangwa mji na mahali na wakati hahudhurii katika mubahala huu kushindana nami na vile vile haachi kuniita kafiri na kunitukana. Amin thumma Amin.³

Enyi wakufurishao, njooni kwenye jambo ambalo ni Sunna ya Mungu na Nabii wake kuwanyamazisha wakufurishao na wakadhibishao. Na kama mkikengeuka mjue kwamba laana ya Mungu iko juu ya wakufurishao ambao kubaki kwao nyuma imedhihirika na hofu yao imeshuhudia kwamba hao ndio waongo.

Mtangazaji:

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

³ Katika tangazo hili Maulamaa wote wanaonikufurisha wamealikwa kwa ajili ya mubahala katika mji wa Amritsar, Dhilkaadi 10, 1310 Hijiria.